Teofilo Kisanji University

TEKU Journal of Interdisciplinary Studies (TJIS)

https://www.teku.ac.tz/tjis.php

MAKALA HALISI

**Kupokelewa:** 1st Des. 2020

**Kurekebishwa:** 28th Juni 2021

**Kukubaliwa:** 30th Juni 2021

**Kuchapwa:** 4th Julai 2021

**Available at**
http://teku.ac.tz/article8.php

# Dhamira za Maradhi, Uganga na Tiba za Asili katika Fasihi Simulizi

Gerephace Mwangosi

Chuo Kikuu Katoliki Ruaha, S.L.P 774, Iringa, Tanzania.

Mawasiliano: mwangosigerephace@yahoo.com

## Ikisiri

Makala haya yameangazia dhamira za uganga, maradhi na tiba za asili katika jamii ya Wanyakyusa. Hoja kuu ilikuwa ni kwamba dhamira hizo zimekuwa na usawili hasi katika nyimbo za Magosi za jamii teule. Ili kuijadili hoja hii, data za msingi za makala haya zilikusanywa mkoani Mbeya katika halmashauri ya Busokelo kwa kurejelea nyimbo za Magosi za jamii ya Wanyakyusa. Data za msingi zilikusanywa kwa mbinu za mahojiano na majadiliano. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika makala haya uliongozwa na nadharia ya Usosholojia. Miongoni mwa matokeo ya makala haya ni kuwa jamii haziwezi kustawi katika harakati za maendeleo yake kama zitaendelea kukumbatia imani za uchawi na ushirikina. Kushamiri kwa imani hizo kunasababisha pia kupuuza jitihada za kisayansi na kisasa za namna bora na sahihi za kupambana na UKIMWI. Aidha, waganga wa tiba za kijadi hawana budi kufanya kazi zao kwa weledi, uaminifu na uadilifu kwa kuzingatia misingi bora ya maarifa na utamaduni uliosheheni masuala yenye tija kwa manufaa ya ustawi wa jamii. Makala haya yanahitimisha kuwa ushauri wa kitaalamu na kiwakati unapaswa kufanyika katika jamii zote hapa nchini ili kukabiliana na maradhi, pamoja na imani za uchawi na ushirikina zilizoshamiri na kuleta maafa katika jamii. Kwa ujumla, haipendezi katika karne hii ya 21 kuamini kuwa nguvu yoyote tusiyoijua ina maana ya ushirikina na uchawi.

**Maneno Msingi:** Maradhi; Uganga; Tiba za Asili; Nyimbo za Magosi; Jamii ya Wanyakyusa

## 1. Utangulizi

Jamii ya Wanyakyusa kama ilivyo katika jamii nyingine hapa nchini Tanzania inao utamaduni wake unaojidhihirisha katika fasihi simulizi. Utamaduni huo ni mapokeo ya vizazi vingi tangu zama za maisha ya mwanadamu katika jamii hiyo (Aswile, 2007 & Wilson, 1957). Nyimbo za Magosi ni utanzu uliotamalaki katika jamii zote zinazoishi nchini Malawi na Tanzania katika ukanda wa ziwa Nyasa (Tew, 1950). Kwa kawaida, nyimbo za Magosi huchezwa na vijana wanaokuwa katika vikundi vinavyokuwa na waimbaji kati ya 8 hadi 15. Kwa kufuata utaratibu waliojipangia, uimbaji wa kawaida hufanyika wakati wa jioni baada ya shughuli za uzalishaji mali na uchumi. Wakati wowote katika msimu wa mwaka huweza kutumika kutegemeana na matukio yanayotokea katika jamii. Mara zote mashidano ya vikundi hufanyika msimu wa kiangazi kuanzia mwezi Julai hadi Oktoba kila mwaka.

Kisanaa, kila kikundi kina upekee katika mitindo ya uimbaji na uchezaji ambao huzidiana. Upekee huzingatia upya wa nyimbo, mitindo ya uchezaji na ubora wa maudhui yaliyomo. Upya na ubora wa maudhui ya wimbo hutakiwa ujitokeze wazi wakati wa uimbaji (Isakwisa, 2003). Mavazi ya msanii huongeza vionjo vya kisanaa sambamba na maudhui. Msanii hulazimika kuvaa mavazi maalum (maleba) ili kuleta uwiano kati ya kile kinachoimbwa na muonekano halisi uliopo katika jamii (Senyamanza, 2015). Mfungamano huo huzifanya nyimbo za Magosi kuthibitisha udhati wa kuwapo kwa uhai wa sanaa ya vitendo. Pia, hujengwa katika uwanja mpana unaolenga kuendeleza misingi iliyokuwapo na iliyopo kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo. Hali na harakati za maisha ya kila siku ya jamii ya Wanyakyusa zimepewa uzito katika uchunguzi na uhakiki wa nyimbo teule. Kwa hiyo, suala la maradhi, uganga na tiba za asili katika nyimbo teule limeshughulikiwa katika makala haya.

## 2. Mbinu, Upeo wa Mada na Nadharia

Makala haya yamechunguza utanzu wa nyimbo za Magosi za jamii ya Wanyakyusa nchini Tanzania. Hoja kuu katika makala haya ni kwamba dhamira ya maradhi, uganga na tiba za asili zimekuwa na usawiri hasi katika nyimbo za Magosi ndani ya jamii ya Kinyakyusa. Aidha, matumizi ya taaluma ya uganga na tiba ndani ya jamii hii hayajapewa kipaumbele stahiki. Hivyo, ili kuijadili hoja hii kwa kina, mwandishi ameshughulikia dhamira ya maradhi, uganga na tiba za asili kwa kurejelea nyimbo teule. Ukusanyaji wa data za uwandani ulifanyika kwa mbinu za mahojiano na majadiliano. Watafitiwa waliohusishwa katika mchakato wa majadiliano na mahojiano ni waimbaji na wapenzi wa nyimbo teule waliopo katika halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya.

Nadharia ya Usosholojia ilitumika katika uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika makala haya. Mojawapo ya misingi yake ni kuichukulia fasihi kuwa ni kitengo pekee kilicho na uwezo wa kuakisi utamaduni wa jamii unaodhibitiwa na miundo ya kijamii (Chimerah na Njogu, 1999). Mtafiti aliichunguza jamii kuwa ni malighafi ya fasihi. Waimbaji wa nyimbo teule waliwekwa katika muktadha wao wa kawaida, ulio wazi na halisi ili kujua mwenendo na shughuli zao kwa kuwa nyimbo zake ni kiungo chake. Kwa hiyo, mjadala wa dhamira teule ulichunguzwa kwa kurejelea uhusiano uliopo baina ya fasihi na jamii kwa kujikita katika nyimbo za Magos iza jamii ya Wanyakyusa.

## 3. Uchambuzi wa Dhamira Katika Nyimbo Teule

### 3.1. Uganga na Tiba Katika Nyimbo za Magosi

Kwa kawaida, hakuna ustaarabu wowote duniani ambao kufikia sasa umejengwa juu ya misingi ya kuiga utamaduni wa jamii na mataifa mengine. Taifa bila utamaduni ni kama taifa bila fahamu (Sengo, 1973). Utamaduni ni kama moyo wa taifa. Kwa msingi huo, tulioko barani Afrika hatuhitaji kuiga falsafa, tabia, mienendo na utamaduni wa watu wengine ili tuwe wastaarabu (Mihanjo, 2010). Kadiri muda unavyopita, ndivyo mazingira ya jamii yanavyobadilika huku baadhi ya mila na desturi zikionekana kupitwa na wakati. Hivyo, msingi wa makala haya ni kuchunguza dhamira ya maradhi, uganga na tiba za asili yanavyoakisiwa katika nyimbo za Magosi za jamii ya Wanyakyusa.

Nyimbo za kijamii ni mojawapo ya vyombo mahsusi vya kijadi vya kijamii vinavyojishughulisha na masuala mbalimbali. Katika makala haya, mtafiti alichunguza uhusiano uliopo baina ya jamii ya Wanyakyusa na mienendo ya shughuli zao za kila siku, falsafa, historia, maendeleo na mitazamo yao kuhusu suala la uganga na tiba kupitia nyimbo zao za Magosi. Nyimbo za Magosi zimesheheni ufafanuzi wa matumizi ya dawa za asili zinazotumika kutibu na kuimarisha afya za wagonjwa. Pia, zinatumika kama dawa mbadala kwa kukinga na kutibu. Nyimbo teule zinatumika kufafanua dhima na matumizi mapana ya dawa za asili katika jamii. Hivyo, jamii hazina budi kuzienzi kwa kuzitumia na kuziendelea kwa maslahi mapana ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

### 3.2. Tiba za Asili Katika Mtazamo wa Ushirikina na Uchawi

Miongoni mwa mikasa mikubwa inayoiandama jamii ya Wanyakyusa na nyinginezo hapa nchini ni kushamiri kwa hisia za imani za uchawi na ushirikina katika jamii hiyo. Suala hilo linaokana kuwa limeshamiri katika jamii mbalimbali za dunia. Kwa mfano, kihistoria, huko Ulaya, maelfu ya watu walipoteza maisha kutokana na kusakwa na kuuawa kwa wale wote waliotuhumiwa kwa uchawi na ushirikina katika jamii. Nchini Ujerumani peke yake inakadiriwa kuwa zaidi ya watu 800,000 waliuawa kwa tuhuma hizo hadi kufikia karne ya kumi na saba (Tehenan, 2003). Katika kipindi hicho, Ulaya pamoja na Marekani walitawaliwa na imani kuhusu uchawi ambapo ilifikia kiwango cha juu kuliko ilivyowahi kutokea katika kipindi chochote hapa Afrika. Jamii ya Wanyakyusa imeshuhudia athari mbalimbali zinazotokana na kuwapo kwa imani za uchawi na ushirikina. Jambo hili linatokana na waganga wa tiba za asili kuhusishwa moja kwa moja na imani za uchawi na ushirikina. Hivyo, jamii hazina budi kuelimishwa kuhusu umuhimu wa tiba za asili katika jamii na mipaka yake baina ya uchawi na ushirikina.

Katika jamii nyingi, upo mtazamo hasi unaowatazama waganga wa tiba za asili kwa jicho la ushirikina na uchawi. Waganga wa tiba asili hutazamwa kama chanzo cha matatizo na migogoro katika jamii nyingi hapa nchini. Hali hii inatokana na udanganyifu unaofanywa na baadhi ya waganga wa tiba za asili wasio waaminifu na waadilifu katika shughuli zao za uganga na tiba, wakiwamo wapiga ramli. Msingi unaoyatazama baadhi ya matukio, hasa vifo vinavyojengwa katika misingi ya imani za kishirikina na uchawi kuwa husababishwa na wataalamu wa tiba za asili (Mwambusye, 2006 & Mwakanjuki, 2011).

Kimsingi, masuala hayo hayana budi kuchunguzwa kwa jicho pevu kwa kuwa huchochea mifarakano na maafa zaidi katika jamii nyingi hapa nchini. Kisayansi na kitaaluma, si vizuri kuamini kuwa kila ugonjwa, vifo ama matatizo yanayotokea katika jamii ni zao la ushirikina na uchawi. Wimbo wa Abalagusi (Waaguzi) unaonesha kuwapo kwa imani za uchawi na ushirikina kama mbinu mojawapo ya kupinga hali ya kuendelea kuamini na kuzifanyia kazi baadhi ya imani zisizo na uthibitisho wa kisayansi zilizotamalaki katika jamii. Wasanii wanaeleza:

| | |
|---|---|
| *Abhalagusi bhikujobha,* | Waaguao wamesema, |
| *Abhaghanga bikujoba,* | Waganga wamesema, |
| *Bhati eghigwe ijini,* | Eti amechukuliwa msukule, |
| *Uju asyele munndeke,* | Huyu aliyebaki mniachie, |
| *Pamo isakundula,* | Labda atakuja kunisaidia, |
| *Mundekele mungangonyola,* | Niachie msiniumize, |
| *Mbelile kangi mbelile,* | Tafadhali tafadhali, |
| *Popapo katumu.* | Sasa inatosha. |

Ubeti huu unaonesha kushamiri kwa imani za kishirikina na uchawi katika jamii ya Wanyakyusa. Jamii ya Wanyakyusa, kama ilivyo katika jamii nyingine hapa nchini, inaamini kwamba uchawi ni teknolojia fiche ambayo haitumiwi kwa manufaa na maslahi mapana ya jamii. Uchawi unatumika vibaya katika nyanja zote za kijamii kwa manufaa ya wamiliki wa teknolojia hiyo (Ntilo, 1972). Wachawi na waganga wa tiba za asili waache tabia ya kutumia vibaya maarifa yao. Jambo hili lina maana kwamba taaluma ya uchawi haina budi kukidhi manufaa na maendeleo ya jamii na taifa ili iwe na tija.

Pia, wasanii hueleza jinsi waganga mahiri wanavyoweza kutibu na kuzuia magonjwa au matatizo yanayoweza kusababishwa na wachawi waletao uharibifu katika jamii zao. Akitoa tahadhari, Guidotti (2010) anaeleza kuwa sio sahihi kuamini kuwa kila linalosemwa na mganga ni uongo au sahihi. Hoja hii inatokana na ukweli kuwa kuna mwachano huru wa kuwapo kwa waganga waaminifu na wasio waaminifu. Ufafanuzi wa Guidotti unawataka waganga wa tiba za asili kufanya kazi zao kwa uaminifu na uadilifu kulingana na misingi ya weledi wa taalimu zao. Pia, hawana budi kufanya kazi zao kwa uaminifu na uadilifu. Kwa kufanya hivyo, taasisi ya tiba za asili, kama tiba mbadala, itaimarika na kuthaminiwa katika jamii na taifa.

Nyimbo za Magosi ni mojawapo ya vyombo vinavyochambua hali halisi kuhusu kuwapo kwa imani za kichawi na kishirikina na matokeo yake katika jamii. Hali ya mauaji ya namna mbalimbali imekuwa ikitokea mara kwa mara katika jamii nyingi hapa nchini. Kiutamaduni, kisheria na ki-haki za binadamu, ni jambo la aibu na unyama uliopindukia kuendelea kuua watu kwa misingi au sababu zozote zile. Katika wimbo wa Mwebaputi (Wachungaji)

viongozi wa kimila na kidini wanaombwa wamuombe Mwenyezi Mungu ili aimarishe ulinzi. Wasanii wanaeleza:

| | |
|---|---|
| *Seluselu jope mundu,* | Albino naye mtu, |
| *Akaleghana nanumwe mwemukughogha,* | Kama muuao mlivyo, |
| *Amuleke ukunfwimisya,* | Acha kumfuatilia, |
| *Ngati bho imbene ja kubhuta,* | Kama mbuzi umchinje, |
| *Mwe bhanyafyale numwe mwebhaputi,* | Machifu na wachungaji, |
| *Tunsume Kyala,* | Tumuombe Mungu, |
| *Seluselu alindililigwe,* | Albino walindwe, |
| *Bhatingibhutigwagha!* | Wasiuawe! |

Ubeti huu unatoa wito kwa viongozi wa ngazi zote za kijamii, wakiwamo wa kimila, kidini na hata serikali ili washikamane kupinga imani potofu zinazochochea mauaji nchini. Kwa hakika, kushamiri kwa imani za kishirikina na uchawi huwafanya watu watumie muda mwingi kushughulikia matatizo hayo badala ya kufanya kazi za uzalishaji mali na uchumi. Hivyo, uchawi na ushirikina husababisha hofu miongoni mwa wanajamii katika maisha na maendeleo yao ya kila siku.

### 3.3. Tiba za Asili Kama Tiba Mbadala

Katika jamii ya Wanyakyusa, suala la uganga na tiba hutazamwa kama tiba mbadala dhidi ya zile za kisasa za hospitalini. Wasanii husisitiza matumizi na kuidumisha taalimu ya tiba za asili kutokana na upana wa dhima zake. Kwa kawaida, baadhi ya magonjwa yanayoshindikana katika hospitali za kisasa hutibiwa kwa kutumia tiba za asili kwa gharama nafuu (Mgogo, 2017). Waganga hao hutoa tiba mbadala kwa kutibu magonjwa sugu yanayoshindikana katika hospitali za kisasa za rufaa zilizotamalaki hapa nchini. Wasanii katika wimbo wa Tiba Mbadala wanaeleza:

Dawa za asili,
Dawa za tangu jadi,
Tangu jadi na sasa,
Ni tiba mbadala,
Waganga wa tiba asilia,
Ni waganga mbadala,
Tuwaenzi!
Tangu kale na sasa,
Hutibu maradhi mengi,
Huponya wengi,
Tuzienzi!

Maelezo haya yanaonesha umuhimu wa kuwapo kwa dawa za asili na waganga wake kwani hutazamwa kama tiba mbadala katika jamii nyingi hapa nchini. Katika baadhi ya vijiji, waganga wa tiba za asili hutegemewa sana katika masuala yote yanayohusiana na tiba za maradhi mbalimbali, ukunga na uzazi. Kwa upande mwingine, tiba za asili huelezwa kuwa zina gharama nafuu, rahisi kupatikana na hazina madhara ambayo ni matokeo kemikali ya matumizi yake. Kimsingi, hutibu maradhi mbalimbali hata yale yaliyoshindikana katika hospitali za kisasa za rufaa zilizotamalaki takribani katika mikoa mingi hapa nchini.

Waganga wanaozungumzwa katika makala haya sio madaktari na wauguzi waliosomea hospitalini. Hawa ni wale wa mitishamba, wafumu, wapiga ramli, wahemba na wanafunzi wao katika shughuli za uganga na tiba za kiasili. Waganga hao hutibu kwa kutumia vitu na mimea ambayo ni dawa. Baadhi ya mimea imeota milimani, makondeni, magengeni, jangwani ama ndani kabisa misituni. Waganga kwa weledi wao huichimba na kuichuma. Mafundi wa uganga na tiba jamii imewafulia msemo kuwa 'Uongo wa mganga nafuu ya mgonjwa' (Nkwera, 2002). Huu ndio msingi wa kuzitazama tiba za asili katika mtazamo chanya. Mtafitiwa mmojawapo anaeleza:

> Kujengwa na kuimarika kwa baadhi ya vituo vya afya na hospitali katika jamii ya Wanyakyusa na kwingineko hapa nchini kumewafanya baadhi ya watu kuanza kupuuza umuhimu na thamani ya waganga wa tiba za asili na dawa zao. Upo ushahidi wa jamii kwamba, baadhi ya maradhi sugu ambayo yamekuwa yakiwasumbua watu kwa muda mrefu, hasa yaliyoshindikana kutibiwa katika hospitali za kisasa yanatibiwa kwa urahisi na waganga wa tiba za asili kwa ufanisi na kwa wakati muafaka. Kwa mfano, katika kijiji cha Ipelo, kata ya Kandete (Halmashauri ya Busokelo) yupo mganga maarufu wa tiba za asili anayejulikana kwa jina la Mwamasimbi. Dawa zake (hukanda kwa kutumia jiwe dogo la mviringo na mafuta ya mbono) zina uwezo wa kuunga na kuinyoosha mifupa iliyovunjika na mgonjwa kurejea katika hali yake ya kawaida kwa muda mfupi. Kwa msingi huo, waganga wa tiba za asili watazamwe kama taasisi maalumu ya tiba mbadala, wasipuuzwe na kutazamwa katika udhaifu na kupitwa na wakati (Mtafitiwa 1: Mahojiano yalifanyika katika kijjiji cha Ipuguso, kata ya Luteba, 18. 04. 2019).

Kipekee, tiba za asili ni mojawapo ya tiba mbadala zinazoweza kusaidia kutibu maradhi tofauti tofauti yakiwamo yale ambayo hayajulikani kwa kutumia vipimo kutoka katika maabara za kisasa. Hata hivyo, waganga hao hawana budi kufanya kazi zao kwa uaminifu na uadilifu kwa kuzingatia weledi na misingi sahihi ya taaluma zao. Kwa kawaida, tiba za asili husaidia kutibu maradhi mengi yaliyoshamiri katika jamii. Tiba za asili na zile za kisasa, kwa kawaida, hutegemeana na hukamilishana (Seitel, 1980). Hivyo, wanajamii wanakumbushwa kuuenzi utamaduni wao, itikadi na falsafa zao, hasa zile zenye tija kwa jamii na taifa lao.

### 3.4. Majukumu ya Tiba za Asili

Fasihi ni chombo kinachohakiki mienendo na harakati za jamii inayohusika. Pia, husawiri kwa undani masuala ya uganga na tiba za asili yanayoendelea katika jamii nyingi hapa nchini, ikiwamo ya jamii ya Wanyakyusa. Fasihi, kupitia nyimbo, imekuwa ikieleza na kuhimiza matumizi ya tiba za asili, umuhimu wake na kutoa mafunzo kuhusu namna sahihi ya kuzitumia. Ufafanuzi huzingatia matumizi ya dawa za asili, ujuzi na uzoefu wa mfumo wa maisha ya jamii ya kijadi ambayo hufuata mazoea ya mila na desturi za jamii hiyo. Kulingana na Seleman (2008), suala la uganga na tiba ni sehemu ya utamaduni wa jamii nyingi zilizopo hapa nchini na kwingineko barani Afrika. Hivyo, kwa kuzingatia maneno ya Seleman, suala hilo halina budi kutumika kwa uaminifu na uadilifu uliojengwa katika misingi imara ya utamaduni wenye tija kwa manufaa ya jamii na taifa.

Katika jamii ya Wanyakyusa, wapo waganga wa tiba za asili wa aina mbalimbali. Baadhi yao ni wataalamu wa tiba za mifugo, binadamu, ukunga na uzazi, magonjwa ya mlipuko na mazindiko ya wanyama na mazao. Pia, wapo wenye uwezo wa kuomba mvua, kutega na kutegua radi na wapiga ramli. Kwa upande mwingine, waganga hao hufanya kazi kama waamuzi wa masuala yanayohusu mila na desturi za jamii kwa kushirikiana na viongozi wa jadi wa maeneo yanayohusika (Mwambusye, 2013). Kwa msingi huo, zipo nyimbo zinazosawiri dhima ya uganga na tiba za asili katika jamii. Katika wimbo wa Imikota gya Kititu (Dawa za Asili) wasanii wanaeleza:

| | |
|---|---|
| *Amwisege,* | Njooni, |
| *Tutindagha abaijholo,* | Tuwashukuru wahenga, |
| *Tumogelege imbatiko syitu,* | Tuenzi tamaduni zetu, |
| *Tusyimikege imbatiko syitu,* | Tudumishe mila zetu, |
| *Tubatike imbatiko syitu,* | Tupange mipango yetu, |
| *Loli syene imbatiko ingolofu,* | Hasa ile ifaayo, |
| *Amwisege,* | Njooni, |
| *Imikota gya kititu kyuma!* | Dawa za asili ni mali! |

Fungu hili linadokeza umuhimu wa kuthamini utaalamu na maarifa ya waganga wa tiba za asili katika jamii. Kimsingi, tiba za asili hazina budi kutazamwa kama tiba mbadala katika jamii. Waganga wa tiba za asili wasitazamwe katika udhaifu. Hii ni kwa sababu uganga na tiba umejengwa katika misingi ya falsafa ya tiba za asili za jamii za Kiafrika (Wilson, 1959). Baadhi ya watafitiwa walizitazama dawa za asili kama tiba mbadala dhidi ya zile za kisasa. Mtazamo huu unatokana na ukweli kuwa baadhi ya magonjwa yanayoshindikana katika hospitali za kisasa hutibiwa kwa mafanikio makubwa kwa kutumia tiba za asili. Hali hii huzifanya jamii nyingi kuuenzi na kuuendeleza uganga na tiba za jadi kwa nadharia na vitendo.

### 3.5. Hali na Suala la Maradhi Nchini

Nyimbo za Magosi katika jamii ya Wanyakyusa zimefungamana kikamilifu na utamaduni wa jamii hiyo. Nyimbo za kijamii ni mojawapo ya vyombo vya kijadi vinavyoihakiki jamii katika nyanja zake zote. UKIMWI ni baadhi ya maradhi yanayoisibu jamii. Mojawapo ya majukumu ya nyimbo za Magosi za jamii ya Wanyakyusa ni pamoja na kuchambua na kuhakiki kwa kina sababu za maambukizi, kuenea kwake, kutoa ushauri na kueleza athari zake kwa jamii na taifa. Pia, nyimbo za Magosi huonesha jitihada zinazochukuliwa na serikali ili kukabiliana na maradhi yanayotokea hapa nchini. Hivyo, wajibu wa jamii ni kuzingatia na kuitikia harakati za serikali za kukabiliana na maradhi yanayokea hapa nchini.

Takwimu za Shirika la Afya la Dunia za mwaka 2015 zinaonesha kuwa asilimia therathini ya vifo vinavyotokana na magonjwa haya vinatokea kwa watu wenye umri chini ya miaka 60 ambayo ndiyo nguvu kazi ya taifa (IPPF, UNAIDS and NAP, 2017). Vifo vinavyosababishwa na maradhi ya UKIMWI vinatokea kwa watumishi wenye umri kati ya miaka 25 hadi 49 na wanaoathirika zaidi katika wizara, idara na wakala za serikali ni wanaume kutokana na wingi wao. Kwa upande wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Serikali za Mitaa wanaoathirika zaidi ni wanawake, hasa walimu, wauguzi na maafisa ugani kwa kuwa wanawake ni wengi zaidi katika makundi hayo kuliko wanaume (Ifakara Health Institute, 2016). Ugonjwa huo kama hautadhibitiwa utaendelea kuathiri ustawi, uendelevu wa jamii na nguvu kazi ya jamii na taifa. Suala la maradhi yanayotokana na suala la UKIMWI limejadiliwa kwa namna mbalimbali katika makala haya.

### 3.6. UKIMWI na Kudhoofika kwa Maadili ya Kiasili

Baadhi ya wasanii wanahusisha suala la kuporomoka kwa maadili na utamaduni wa kiasili katika jamii nyingi hapa nchini na kuwapo kwa kasi ya maambukizi ya UKIMWI. Kudhoofika kwa harakati za mafunzo ya kijadi kupitia jando na unyago katika baadhi ya jamii pia kumechangia kuenea kwa UKIMWI. Mafunzo ya jando na unyago yaliwaingiza kikamilifu wanafunzi waliohusika katika ulimwengu wa maisha ya mapenzi na ndoa katika hali ya ukomavu wa kimwili na kiakili. Hata hivyo, uchunguzi wa kina hauna budi kufanywa ili kuthibitisha hoja hiyo. Mjengwa (2012:14) anaeleza:

> Sababu za kuvunjika kwa utamaduni wa kiasili zilichangia sana kuenea kwa UKIMWI kwa kuwa ilikuwa vigumu kwa vijana waliofundwa kikamilifu katika jando na unyago kuingia na kujitumbukiza kwenye uhusiano wa kimapenzi kwa urahisi.

Maelezo ya hapo juu yanaonesha kuwa misingi ya elimu ya kiasili kupitia jando na unyago ilisaidia kuwaimarisha vijana kuyakabili mazingira yao kikamilifu. Harakati za jando na unyago zimechangia kuwaingiza, kuwashirikisha na kuwajenga vijana katika misingi ya awali ya kimaadili ya jamii zao. Mtindo wa kuiga mila na desturi za kigeni unatazamwa kama njia mojawapo iliyochangia kasi ya kumong'onyoka kwa maadili ya kijamii (Mutembei, 2006). Hivyo, jamii haina budi kuiga mila na desturi zenye tija na kuachana na zile zote zisizo na tija. kwa manufaa endelevu ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

Kwa upande mwingine, wakazi wa vijijini wanaiangalia miji kama sehemu iliyoporomoka kimaadili, hasa kuhusu mienendo ya vijana na matokeo yake. Mmomonyoko wa maadili umesababishwa na utamaduni mseto uliotamalaki katika jamii zetu (Seleman, 2008). Utamaduni huo umechangia kuitumbukiza jamii katika maambukizi ya UKIMWI. Harakati za vijana za kukimbilia mijini zinahusishwa moja kwa moja na kasi ya kuongezeka kwa maambukizi zaidi katika jamii. Wasanii wanaihimiza jamii kubadili tabia na kufuata ushauri unaotolewa na wataalamu kuhusu namna bora ya kuepuka maambukizi zaidi ya UKIMWI. Wasanii katika wimbo wa Tukumalika (Tunakwisha) wanaeleza:

| | |
|---|---|
| *Twitike!* | Tukubali! |
| *Twitike simalike,* | Tukubali yaishe, |
| *Abamang'anyi,* | Wataalamu, |
| *Batwele amasisa,* | Wameletea mashudu, |
| *Batwele ifisyesye,* | Wameleta mikate, |
| *Tulye tujeko,* | Tule tuishi, |
| *Tukongege imbatiko,* | Tufuate taratibu, |
| *Kongaga ingomelesyo,* | Ushauri wa waganga, |
| *Tusanusye akajilo!* | Tubadili tabia! |

Nukuu hii inaonesha hali na matokeo ya UKIMWI kwa Wanyakyusa na katika jamii nyingi hapa nchini. Pia, wanaonesha kuwapo kwa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI zinazojulikana kama Antiretroviral (ARV). Jamii haina budi kuzitumia dawa hizo kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya. Kuwapo kwa dawa hizo isiwe kigezo cha jamii kujisahau na kupuuza jitihada za kupambana na UKIMWI. Hivyo, matumizi ya dawa za

kupunguza makali ya UKIMWI yawe sambamba na harakati za kupambana na kuyakabili maambukizi zaidi.

Kihistoria, Afrika ilivamiwa na taasisi nyingi za kigeni zilizoathiri kwa kiasi kikubwa utamaduni wa kiasili. Waafrika sasa wamekuwa watumwa wa mila na tamaduni za kigeni katika ngazi zote za maisha na maendeleo yao. Hali ya kuiga utamaduni wa kigeni, kiasi kikubwa, imechangia kuvunjika kwa maadili ya kijamii (Mwabukusi, 2014). Hali hiyo imesababisha kasi ya kuenea kwa UKIMWI kutokana na kuiga mitindo ya maisha na baadhi ya tabia za kigeni zisizostahili, zikiwamo zinazoruhusu ushoga, ulevi, umalaya na uasherati zimechangia kuwapo kwa kasi ya maambukizi nchini.

### 3.7. Umalaya Kama Wakala wa UKIMWI

Umalaya na uasherati ni kama wakala ama mojawapo ya vyanzo vya kuenea kwa kasi ya maambukizi ya UKIMWI katika jamii nyingi hapa nchini na kwingineko Afrika. Umalaya ni kitendo cha mwanaume au mwanamke mwenye tabia ya uzinzi (TUKI, 2004). Pia, huelezwa kuwa ni mwanamke anayejiuza kwa ajili ya kupata fedha. Wasanii katika wimbo wa Tukumalika (Tunaisha) wanakemea tabia ya umalaya ili kuepuka maambukizi zaidi katika jamii. Wasanii wanaeleza:

| | |
|---|---|
| *Ubukokonyale,* | UKIMWI, |
| *Ngwego kubatubwa,* | Mkuki kwa vijana, |
| *Jimalile abandu,* | Unamaliza watu, |
| *Twikete utujilo,* | Tubadili tabia, |
| *Tuleke uboloki,* | Tuache umalaya, |
| *Uboloki bukugoga,* | Umalaya unaua! |

Kimsingi, umalaya unatazamwa kuwa nyenzo kuu inayosababisha kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Nukuu hii inaitaka jamii ibadili tabia kwa kuacha tabia za uzinzi na uasherati kama njia mojawapo ya kuepukana na kasi ya maambukizi. Kukosekana kwa uaminifu katika suala la mapenzi na ndoa ndiyo msingi wa kuongezeka kwa kasi ya maambukizi ya UKIMWI katika jamii (Chamba, 2011). Kwa hiyo, suala la kuimarika kwa uaminifu miongoni mwa wanajamii halina budi kutazamwa kama nguzo muhimu dhidi ya mapambano ya UKIMWI katika jamii zote hapa nchini.

### 3.8. Ndoa za Mitara na UKIMWI

Kukosekana kwa uaminifu katika ndoa za mitara ni miongoni mwa sababu za kuongezeka kwa maambukizi ya UKIMWI. Suala la mitara katika jamii ya Wanyakyusa linatazamwa katika ncha mbili. Kwanza, kama alama ya umaarufu na utajiri. Kwa kawaida, maskini hana uwezo wa kumudu kuisimamia familia zaidi ya moja. Pili, kama ishara ya kutoridhika kimapenzi. Kwa upande mwingine, makala haya yanatambua kuwapo kwa baadhi ya miongozo ya kidini inayoruhusu kuwa na mke zaidi ya mmoja kulingana na misingi ya imani zao. Katika makala haua, suala hili limechunguzwa kwa mtazamo wa kijadi katika jamii ya Wanyakyusa. Kwa mujibu wa mtazamo uliodokezwa, kimila, kuoa wanawake wengi ni sehemu ya umaarufu na utajiri. Wasanii katika wimbo huo huo wa Tukumalika (Tunaisha) wanadokeza madhara yake katika jamii yao:

| | |
|---|---|
| *Ntubwa,* | Kijana, |
| *Amatala,* | Mitara, |
| *Ubwelefu bwan kifwani,* | Umaarufu wa bandia, |
| *Ikinyony kikugoga,* | Tamaa yakuponza, |
| *Mmatala ulwijisyo nalumo!* | Mitara haina uaminifu! |

Kwa mtazamo wetu, mitara si tatizo kama suala la uaminifu na mshikamano litaimarika miongoni mwa wanandoa. Kasi ya maambukizi ya UKIMWI imekuwa kubwa zaidi kutokana na kukosekana kwa uaminifu katika ndoa za mitara. Hoja hii inapewa nguvu na TACAIDS (2007) kwamba kundi la wanawake ndilo linaloongoza kuathirika zaidi kutokana na kushamiri kwa mila na desturi ambazo hazina tija, zikiwamo za kurithi wajane. Mhojiwa mmojawapo anaeleza:

> Licha ya kuwapo kwa elimu kuhusu maambukizi ya virusi vya UKIMWI na madhara yake ambayo yameshuhudiwa takribani katika kila kaya ya Mnyakyusa, bado jamii inamtazama mwanamke kama chanzo cha maambukizi ya UKIMWI. Hii ni mojawapo ya mitazamo inayosababisha kufifiza jitihada za kupambana na maambukizi zaidi. Kuendelea kumlaumu mwanamke ni jambo linalodhoofisha harakati za mapambano makali dhidi ya UKIMWI. Ili kuondokana na tatizo hilo, lazima jamii iyatazame masuala haya kwa jicho pana zaidi badala ya kuyachunguza kwa mtazamo finyu na upekee wa mtu mmoja au kikundi fulani katika kijamii (Mtafitiwa 2: Mahojiano yalifanyika katika kijjiji cha Ikubo, kata ya Luteba, 23. 04. 2019).

Kipekee, suala la maambukizi ya UKIMWI halina budi kutazamwa kwa uyakinifu kulingana na hali halisi ya vyanzo vya maambukizi na jitihada zinazolenga kuyatokomeza. Jitihada za kuukabili UKIMWI hazina budi kuanzia katika ngazi ya kaya badala ya kuwalenga watumishi wa umma pekee, hasa wanaoishi katika miji mikubwa hapa nchini. Aidha, wale wanaoishi katika miji mikubwa wanatazamwa kama wana mwamko mkubwa kuhusiana na elimu ya maambukizi ya UKIMWI wakilinganishwa na wale wanaoishi sehemu za vijijini. Hata hivyo, uwiano uwapo katika harakati za kuyakabili maambukizi zaidi. Vita vya UKIMWI havina budi kulenga vyanzo mahsusi vya maambukizi.

### 3.9. Kinga na Tiba ya UKIMWI

Makala haya yamebaini kuwapo kwa nyimbo za Magosi zinazoonesha jitihada za wataalamu wa afya jinsi wanavyokabiliana na VVU. Mashudu ni machicha yanayopatikana baada ya kukamua mafuta ya alizeti au pamba yanayotumika kulishia wanyama; na huwafanya wanyama hao wanenepe zaidi. Mashudu yanalinganishwa na dawa za ARV anazopata mwathirika ili kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI. Pia, huonesha matumaini kwa mwathirika kuishi zaidi baada ya kupata dawa za kupunguza makali. Kuendelea kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI kusichangie maambukizi zaidi. Wimbo wa Tukumalika (Tunaisha) unaonesha wazi kukosekana kwa tiba ya UKIMWI. Wasanii wanaeleza:

| | |
|---|---|
| *Ubhukokonyale ubho tata,* | UKIMWI huo baba, |
| *Bhukumalile abhandu,* | Unamaliza watu, |
| *Twikete utujilo,* | Tubadili tabia, |
| *Tuleke ubholoki,* | Tuache umalaya, |

| | |
|---|---|
| *Tunsighile ubhukokonyale,* | Tuzuie UKIMWI, |
| *Gukana nkota!* | Hauna tiba! |

Kukosekana kwa tiba sahihi kama inavyoelezwa na wataalamu wa afya kumesababisha kuibuka kwa waganga wanaojaribu kutibu kwa kutumia dawa za kiasili. Licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na waganga wa tiba asilia, akiwamo Ambilikile Mwasapile (mchungaji), hakuna wagonjwa waliothibitishwa kitaalamu kupona kabisa (Mjengwa, 2012). Dawa yake ilisifika kwa jina la 'Kikombe cha Babu' ilitengenezwa kwa mti wa Mugariga. Watu kutoka sehemu mbalimbali za nchi na kwingineko Afrika Mashariki waliifuata huko Loliondo Arusha, mwanzoni mwa miaka ya 2000. Baadhi ya watu wanaonesha kukosa imani kuhusu harakati za waganga wa tiba za asili katika jitihada za kupambana na UKIMWI. Mtafitiwa mmojawapo anaeleza:

> Jamii inahitaji kupewa elimu kamili kuhusu maambukizi ya UKIMWI na matibabu yake. Maangamizi zaidi yataendelea kushuhudiwa katika jamii kama imani itajengwa katika misingi ya kuziamini zaidi tiba za asili pekee na kupuuza kabisa za kisasa. Kuwapo kwa tiba za asili kutazamwe kama mojawapo ya jitihada za kutafuta tiba na kupambana na UKIMWI. Kwa mfano, licha ya waathirika wengi kufanya jitihada na kutumia gharama kubwa za kutibiwa kwa waganga wa tiba za asili, bado maafa yanaendelea kila kukicha katika jamii yetu. Jambo la msingi ni kwamba, jamii ielimishwe kuhusu namna sahihi ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI (Mtafitiwa 3: Mahojiano yalifanyika katika kijjiji cha Mpunguti, kata ya Luteba, 13. 04. 2019).

Jambo la heri ni kwamba, jamii inaamini kuwa UKIMWI hauna tiba licha ya kuwapo kwa jitihada kubwa zinazofanywa na waganga wa tiba za asili na za kisasa. UKIMWI hauna tiba na hauchagui mkubwa wala mdogo (Pastore, 1993). Baadhi ya wanajamii wanauhusisha UKIMWI na janga linalohusishwa na uchawi ulioletwa ili kuiangamiza jamii. Katika baadhi ya jamii bado UKIMWI unahusishwa na imani za kishirikina na ushetani (Mutembei, 2009). Kwa hiyo, kuwapo kwa imani hizo kunadhoofisha jitihada za msingi za kupambana na maambukizi zaidi.

Kwa namna hali inavyoendelea, wanafasihi hawajabaki nyuma katika kushughulikia matatizo mbalimbali yanayoisibu jamii kwa kuwa hulazimika kukemea na kuielimisha jamii kupitia kazi zao za kisanaa. Wengi hutumia kalamu zao ili kuielimisha jamii. Wanjala (2013) anaishambulia jamii na kuikemea kutokana na kukithiri kwa mauaji ya Albino yanayoendelea nchini. Anaeleza:

Mlemavu wa ngozi, hakupenda hali hiyo,
Hayo mambo ya Mwenyezi, vipi umfanyie ukatili,
Mwawauwa kama wezi, eti utajiri kuupata,
Albino muwatendeavyo, ni unyama usiofaa.

CHAWAKAMA tumia kalamu, kuielimisha jamii,
Mauaji si ubinadamu, tutokomeze hali hii,
Kuua tendo halamu, tulipinge kwa bidii,
Albino muwatendeavyo, ni unyama usiofaa.

Maelezo hayo hapo juu yanaonesha ukatili unafanywa dhidi ya walemavu wa ngozi. Suala la ushirikina na uchawi linaonekana kuchukua nafasi kubwa kuchochea ukatili unaofanywa katika jamii. Kwa hakika, kushamiri kwa imani za kishirikina na uchawi huwafanya watu watumie muda mwingi kushughulikia matatizo hayo badala ya kufanya kazi za uzalishaji mali na uchumi. Uchawi na ushirikina husababisha hofu miongoni mwa wanajamii katika maisha yao ya kila siku.

## 4. Hitimisho

Makala haya yameangazia masuala ya uganga, magonjwa na tiba za asili katika jamii ya Wanyakyusa. Hoja kuu ilikuwa ni kwamba dhamira hizo zimekuwa na usawili hasi katika nyimbo za Magosi za jamii teule. Makala haya yamebainisha wazi kuwa jamii haiwezi kustawi katika harakati za maendeleo yake kama itaendelea kukumbatia imani za uchawi na ushirikina. Kwa upande mwingine, waganga wa tiba za kijadi hawana budi kufanya kazi zao kwa weledi, uaminifu na uadilifu kwa kuzingatia misingi bora ya taaluma zao. Ushauri wa kitaalamu unahitajika ili kukabiliana na maradhi, pamoja na imani za uchawi na ushirikina zilizoshamiri na kuleta maafa katika jamii. Kushamiri kwa imani hizo kunasababisha pia kupuuza jitihada za kisayansi na kisasa za namna bora na sahihi za kupambana na UKIMWI. Hatima ya ustawi na uendelevu wa kizazi cha leo itakuwa mashakani kama jamii itaendelea kuamini kwa vitendo imani za ushirikina na uchawi. Kwa ujumla, haipendezi katika karne hii ya 21 kuamini kuwa nguvu yoyote tusiyoijua ina maana ya ushirikina na uchawi.

## Ufadhili

Hakuna.

## Migogoro ya Kimasilahi

Mwandishi wa Makala haya anatamka kwamba hakuna mgongano wa kimasilahi wowote utakaoweza kutokea kutokana na kuchapishwa kwa makala haya katika Jarida hili. Utafiti ulifanyika kwa jitihada za mwandishi mwenyewe pasipo malipo kutoka kwa mtu au shirika lolote.

## Shukrani

Makala haya ni matokeo ya utafiti uliofanywa katika jamii ya Wanyakyusa wa Busokelo Mkoani Mbeya. Mwandishi anashukuru kwa mchango uliotolewa na watoa habari wote katika utafiti uliofanyika. Asante sana!

## Marejeleo

Aswile, A. (2007). An Examination of Language Use in the Bhanyakyusa Wedding Songs. A Thesis for Bachelor Degree, University of Dar Es Salaam.

Chamba, L. A. (2011). Dhamira Kwenye Nyimbo za Wasanii Wasioona na Mtazamo kwa Jamii. Tasinifu Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Guidotti, R. (2010). *Map of Albinism World Wide*. New York, USA.

Ifakara Health Institute (2016). *Draft Report on Heterosexual Anal Intercourse*. Dar Es Salaam: TACAIDS.

IPPF, UNAIDS and NAP, (2017). *People Living with HIV Stigma Index.* Dar Es Salaam: IPPF, UNAIDS and NAP.

Isakwisa, C. (2003). Nyimbo za Harusi za Wanyakyusa na Mabadiliko ya Jamii. Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Mgogo, Y. P. (2012). Matumizi ya Nyimbo za Wanyiha Misibani. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mihanjo, A. (2010). *Falsafa na Ufunuo wa Maarifa*. Morogoro: Turiani.

Mjengwa http://mjengwa blog.com.

Mutembei, A. K. (2006). 'Nadharia ya UKIMWI katika Fasihi Andishi: Mifano Kutoka Kwenye Mashairi'. Katika Sewangi, S.S., na Madumulla, J. S., (2005), *Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI,* Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Mutembei, A. K. (2009). *UKIMWI katika Fasihi ya Kiswahili 1982 - 2006*. Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam: TATAKI.

Mwabuka, M. (2013). The Changing Roles of Banyakyusa Oral Poetry in the Contemporary Setting. A Thesis of a Doctor of Philosophy, Open University of Tanzania.

Mwabukusi, A. (2014). Nyimbo za Kazi katika Jamii ya Wanyakyusa. Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji.

Mwakanjuki, N. (2011). Athari za Mabadiliko ya Kijamii na Kiuchumi katika Nyimbo za Kapote za Mwimbaji Mwandwanga katika Jamii ya Wanyakyusa. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mwambusye, D. (2006). *A Guide to Nyakyusa Cultural Heritage*. Tukuyu: Tukuyu Highland Press.

Mwambusye, D. (2013). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kinyakyusa*. Tukuyu: Tukuyu Highland Press.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F. V. (2002). *Fasihi simulizi, Tamrini za Sekondari na Vyuo*. Dar Es Salaam: Busness Printers Limited.

Ntilo, S. J. (1972). *Desturi za Wachaga*. Nairobi: General Printers Darlington Road.

Pastore, L. J. (1993). *Comfroting AIDS through Literature*. University of Illnois. USA.

Seitel, P. (1980). *See so that We May See: Performances and Interpretations of Traditional Tales from Tanzania.* Bloomington: Indiana Press.

Seleman, H. J. (2008). Ujamiishaji wa Kijinsia katika Nyimbo za Harusi za Kihaya. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Sengo. T. S. Y. (1973). *Fasihi Simulizi ya Mtanzania Hadithi*. Dar Es Salaam: Dar Es Salaam University Press.

Senyamanza, C. A. (2015). Tathmini ya Mabadiliko ya Rara Mintarafu Maendeleo ya Jamii: Uchunguzi katika Mkoa wa Songwe. Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TACAIDS. (2007). http://tanzania.go.tz/pdf/sera ya ukimwi.pdf.

Tehenan, M. (2003). *Maisha na Mafanikio*. Dar Es Salaam: Jitambue Media Co. Limited.

Tew, M. (1950). *People of the Lake Nyasa Region*. London: SAGE.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar Es Salaam: TUKI.

Wanjala, S. F. (2013). *Kitovu cha Fasihi Simulizi: Kwa Shule, Vyuo na Ndaki.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Wilson, M. (1957). *Rituals of Kingship Among the Nyakyusa*. International African Institute: Oxford University Press.

Wilson, M. (1959). *Communal Rituals of the Nyakyusa. An Account of the Impact of Colonial Rule and Christian Teaching on the Nyakyusa Society and eliefs*. London: Oxford University Press.

## Wasifu wa Mwandishi



**GEREPHACE MWANGOSI** alizaliwa katika Halmashauri ya Busokelo, wilaya ya Rungwe, mkoa wa Mbeya nchini Tanzania. Alitunukiwa Shahada ya Kwanza ya Sanaa katika Elimu (2006) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili na Shahada ya Uzamivu katika Falsafa (2019) zote mbili kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Alifanya kazi kama Mhadhiri Msaidizi katika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Ndaki ya Mbeya. Hivi sasa, Dkt. Mwangosi ni Mhadhiri wa Mafunzo ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha kilichopo Iringa. Amechapisha makala na vitabu katika nyanja za Kiswahili na Utafiti.

Jinsi ya kuyarejea makala haya: Mwangosi G. (2021). Dhamira za Maradhi, Uganga na Tiba za Asili katika Fasihi Simulizi. *TEKU Journal of Interdisciplinary Studies, 1*(1), 59–65.